# Mpango wa Uboreshaji na Ufuatiliaji wa Kusoma ni nini?

Mpango wa Uboreshaji na Ufuatiliaji wa Kusoma, ambao wakati mwingine huitwa RIMP, ni hati ambayo shule hutumia kufuatilia jinsi zitakavyotegemeza mtoto na stadi za kusoma na kuandika ikiwa mtoto hapati alama au hazidi alama fulani kwenye mtihani wa uchunguzi wa kusoma wa darasa lake. Mpango huu huanzia Chekechea. Unaweza kuona Mfano wa Kiolezo cha RIMP mtandaoni.

Kwa mujibu wa sheria, shule zote za umma kule Ohio lazima ziunde Mpango wa Uboreshaji na Ufuatiliaji wa Kusoma kwa mwanafunzi ambaye hafikii matarajio (anasoma chini ya kiwango cha darasa), ndani ya siku 60 baada ya kupokea matokeo ya uchunguzi wa kusoma. Hii ni sehemu ya sheria ya ya Ohio Hakikisho la Kusoma la Darasa la Tatu (Angalia Kanuni Iliyorekebishwa ya Ohio 3313.608).

## Je, jukumu langu kama mzazi/mlezi ni gani kuhusiana na Mpango wa Uboreshaji na Ufuatiliaji wa Kusoma?

1. **Mpango huu ni fursa kwako kufanya kazi pamoja na shule.** Wilaya yako ya shule inahitajika kisheria kukuhusisha wewe na mwalimu wa darasa la mtoto wako katika kuandaa mpango huo. Mpango huo unapaswa kuorodhesha usaidizi wa kusoma na kuandika ambao mtoto wako atapokea. Usaidizi ulioorodheshwa katika mpango huo unapaswa kutegemea data ya kusoma na kuandika ya mtoto wako, na maoni yako kuhusu jinsi mtoto wako anavyojifunza vyema zaidi.
2. **Mpango huo ni hati iliyoandikwa, ambayo itakusaidia kufuatilia maendeleo ya mtoto wako na usaidizi unaotolewa na shule kwa muda.** RIMP itaendelea kusasishwa na kutumika katika taaluma ya kielimu ya mtoto wako ya K-12 hadi atakaposoma katika kiwango cha gredi.
3. **Kwa kuwa mpango huo unaonyesha waziwazi ujuzi ambao mtoto wako anahitaji kuboresha, unaweza pia kumsaidia mtoto wako kufanya mazoezi ya stadi hizo nje ya saa za shule.**

**Mfano**

Matokeo ya Mtihani wa Uchunguzi wa Kusoma ya mtoto yanaonyesha kuwa anahitaji usaidizi zaidi wa kusoma sauti za kwanza kwa maneno. Mpango (RIMP) wa kumsaidia mtoto unaandikwa na kushirikishwa na wazazi wa mtoto.

-----

Mwalimu na wazazi hukutana na kila mmoja wao hushiriki maoni ya mpango huo, kuhusu jinsi ya kumsaidia mtoto katika kufanya mazoezi ya sauti na herufi hizo wakati wa siku ya shule. Pia wanapanga ni lini watakagua tena stadi za mtoto na kuzungumza tena.

-----

Shule hufanya mabadiliko kwenye mpango huo ili kujumuisha kile walichozungumzia katika mkutano na wazazi na kutuma nakala ya mpango huo kwa familia.

Mtoto wako atakuwa na Mpango wa Uboreshaji na Ufuatiliaji wa Kusoma hadi atakaposoma katika kiwango cha gredi. Wanafunzi wanaweza kuwa na RIMP hadi gredi ya 12. Shule pia zinaweza kuunda RIMP kwa wanafunzi ikiwa kuna ushahidi unaoonyesha kwamba mwanafunzi anahitaji usaidizi katika kusoma, hata kama atapata alama zaidi ya kiwango cha gredi mwanzoni mwa mwaka.

**Je, Una Maswali?** Tuma barua pepe kwa ThirdGradeGuarantee@education.ohio.gov.

Ohio Statewide Family Engagement Center at The Ohio State University

Ohio Department of Education & Workforce